

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 44 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** OKTOBA 2024

MHE. ZAINAB TSC ENDELENI KUSIMAMIA MAADILI YA WALIMU

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Mhe. Zainab Katimba akifungua mafunzo yakuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati za Wilaya za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kutekeleza majukumu yao tarehe 25 Septemba, 2024 jijini Dar es Salaam.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

MAFUNZO YA KAMATI ZA WILAYA YASAIIDIE KUONDOA DOSARI KATIKA KUSHUGHULIKIA MASHAURI YA NIDHAMU YA WALIMU

Hivi karibuni Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) iliendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati za TSC ngazi ya Wilaya Nchi nzima kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji kazi hususan katika kushughulikia mashauri ya nidhamu ya walimu.

Mafunzo hayo yalifanyika katika Kanda tano (5) ambapo kitaifa yalifunguliwa tarehe 25 Septemba, 2024 na Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Zainabu Katimba (Mb) na kufungwa tarehe 26 Septemba, 2024 na Katibu Mkuu OR – TAMISEMI, Adolf Ndunguru.

Katika nyakati tofauti viongozi hao wamesisitiza wajumbe wa kamati hizo kuhakikisha wanazingatia Sheria, Kanuni,

Taratibu na Miongozo mbalimbali iliyopo wakati wa kutekeleza majukumu yao ili waweze kutenda haki kwa walimu.

Rai yetu ni kwamba elimu iliyopatikana katika mafunzo hayo isaidie kila mjumbe kuondoa dosari zilizokuwa zinajitokeza mara kwa mara katika kushughulikia mashauri ya nidhamu kwa walimu ili kuhakikisha haki inatendeka na kupesha hasara kwa Serikali pale inapobainika mwalimu hakutendewa haki wakati wa uendeshaaji wa shauri lake katika ngazi ya Wilaya.

Vilevile, tunatoa pongezi kwa Menejimenti ya TSC chini ya Katibu wake, Mwl. Paulina Nkwama kwa kuona umuhimu wa kuwajengea uwezo wajumbe hao ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

KATUNI



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Richard L. Odongo
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya

Mhariri Mkuu

Artemony T. Vincent

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**



MHE. ZAINAB TSC ENDELENI KUSIMAMIA MAADILI YA WALIMU

**Na Mwandishi wetu – TSC,
Dar es Salaam.**

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Mhe. Zainab Katimba (Mb) ameitaka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kuendeleza jukumu lake la msingi la usimamizi wa utumishi na Maadili ya Walimu.

Ametoa kauli hiyo tarehe 25 Septemba, 2024 wakati akifungua mafunzo ya siku mbili kwa niaba wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa (Mb) ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati za Wilaya za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kutekeleza majukumu yao.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuwa na walimu wenye kujituma na wanaozingatia maadili ya kazi yao kwa ajili ya kuwalea Watoto kwa usahihi na hivyo kuboresha elimu nchini.

Mhe. Zainab aliwataka washiriki kutumia mafunzo yenye mada zinazohusu Muundo na Majukumu ya Tume, Majukumu ya Kamati za Wilaya pamoja na taratibu katika ushughulikiaji wa mashauri ya nidhamu na Rufaa kwa Walimu kuwa chachu ya kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu ya kila siku ya Tume na Serikali kwa ujumla.

Alielekeza kuwa baada ya mafunzo hayo kila mhusika anapaswa kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyopo na kutenda haki kwa walimu.

“Naomba nirudie kuipongeza Tume kwa kazi nzuri mnayoifanya... Naomba sote kwa pamoja tuendeleo kutekeleza kauli mbiu ya “Kazi iendeleo”. Kauli mbiu hii



Katibu Tawala Mkoa wa Dar es Salaam, Dkt. Toba Nguvula akitoa salamu za Mkoa tarehe 25 Septemba, 2024 wakati wa halfa ya ufunguzi wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati za Wilaya za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa Kanda ya Mashariki.

naomba itekelezwe kwa ufanisi na uadilifu na sisi kama Serikali tutaendelea kuwa pamoja nanyi katika kuhakikisha kwamba tunatoa ushirikiano wa kutosha,” alisisitiza.

Aidha, Mhe. Zainab alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa juhudi za kuhakikisha kuwa, Wizara na Taasisi zinazosimamia Utumishi wa Walimu zinaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzipatia fedha, nyenzo na watumishi wenye ujuzi na weledi wa kutosha ili kuboresha Sekta ya Elimu Nchini.

Awali, Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Hadi Muruke alisema kuwa Mafunzo hayo ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati za Wilaya yanafanyika katika Kanda mbalimbali ambapo Kanda ya Kaskazini imehusisha mikoa ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro na Tanga huku Kanda ya Mashariki ikihusisha mikoa ya Lindi, Mtwara, Dar es Salaam, Pwani na Morogoro.

Alisema kuwa kwa Kanda ya Kati mafunzo hayo yanahusisha Wilaya za mikoa ya Kigoma, Katavi, Tabora, Singida na Dodoma; Kanda ya Ziwa ina mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Geita; na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini mafunzo hayo yanajumuisha wilaya za mikoa ya Rukwa, Songwe, Ruvuma, Njombe, Iringa na Mbeya.

Kwa upande wa Katibu Tawala Mkoa wa Dar es Salaam, Dkt. Toba Nguvula alisema kuwa Walimu wanamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa juhudi zake za kuhakikisha anatutua changamoto mbalimbali ambazo zilikuwa zikiwakabili walimu ikiwemo za kuwapandisha madaraja.

Aliwataka Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu kuhakikisha wafanyakazi kwa juhudi katika kumsaidia Rais kwenye usimamizi wa nidhamu, mashauri na madaraja kwa walimu kwa ajili ya maendeleo ya Nchi.



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Mhe. Zainab Katimba (kushoto) akibadilishana mawazo na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu Prof. Masoud Muruke (kulia) kabla hajafungua mafunzo ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati za Wilaya za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tarehe 25 Septemba, 2024 jijini Dar es Salaam.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitambulisha washiriki wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati za Wilaya kwa Kanda ya Mashariki tarehe 25 Septemba 2024, jijini Dar es Salaam.



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Mhe. Zainab Katimba (katikati) akibadilishana mawazo na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu Prof. Masoud Muruke (kulia) na Katibu wa Tume Mwl. Paulina Nkwama kabla hajafungua mafunzo ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati za Wilaya za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tarehe 25 Septemba, 2024 jijini Dar es Salaam.



Baadhi ya Washiriki wa Mafunzo ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati za Wilaya za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ili kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yao wakiwa katika mafunzo hayo tarehe 25 Septemba, 2024 jijini Dar es Salaam.



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Mhe. Zainab Katimba (kushoto) akibadilishana marwazo na Katibu wa Tume Mwl. Paulina Nkwama wakati wa hafla ya ufunguzi wa mafunzo ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati za Wilaya za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tarehe 25 Septemba, 2024.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Mhe. Zainab Katimba (katikati) akishiriki sala ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tarehe 25 Septemba, 2024 wakati wa hafla fupi ya ufunguzi wa mafunzo ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati za Wilaya za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) katika kutekeleza majukumu yao.



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Mhe. Zainab Katimba (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya Wajumbe wa Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu na Watumishi wa Tume Makao Makuu tarehe 25 Septemba, 2024 baada ya kufungua mafunzo ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati za Wilaya za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kutekeleza majukumu yao.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Mhe. Zainab Katimba (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 25 Septemba, 2024 baada ya kufungua mafunzo yakuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati za Wilaya za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kutekeleza majukumu yao.

UONGOZI INSTITUTE YAWAFUNDA MENEJIMENTI YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU

**Na Mwandishi Wetu-TSC-
Arusha**

Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute) imeendesha mafunzo kwa Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ya kuwajengea uwezo kuhusu masuala mbalimbali ya kiuongozi ili waendeleo kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Akifungua mafunzo hayo tarehe 9 Septemba, 2024 Jijini Arusha Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama alisema kuwa mafunzo hayo yamelenga kuwajengea uwezo Menejimenti ambapo mada mbalimbali zitatolewa ikiwemo Akili Tafukuri (Personal Leadership and Emotional Intelligence) na Uongozi wa Kimkakati (Strategic



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo Menejimenti ya TSC tarehe 9 Septemba, 2024.

Leadership).

Alisema kuwa mada nyingine ni Uhusiano na Mawasiliano ya Mkakati, Uongozi na Utawala

katika Sekta ya Umma, Maadili kwa Viongozi na Usimamizi wa Kimkakati wa Rasilimali za Umma.

Mwl. Paulina alisema kuwa mara baada ya mafunzo hayo Menejimenti kwa kushirikiana na Watumishi waliopo chini ya Idara na Vitengo vyao watasaidia kutoa huduma kwa ufanisi kwa wadau wake wakiwemo walimu.

Aliongeza kuwa mafunzo hayo ni maalumu kwa ajili ya kuiwezesha Menejimenti ya Tume kuwa na usimamizi mzuri wa Ofisi za Tume ngazi ya Wilaya.

Kwa upande wa Mratibu wa Mafunzo kutoka Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute), Emmanuel Tessua alisema kuwa wanaendesha kozi mbalimbali za kuwajengea viongozi uwezo ili waweze kutoa huduma nzuri kwa wananchi.

Aliongeza kuwa Taasisi hiyo pia imekuwa ikitoa Postgraduate Diploma ya Uongozi na kozi Maalum kwa Wanawake inayolenga kuwajengea uwezo katika masuala ya uongozi.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama (katikati waliokaa) akiwa na Wajumbe wa Menejimenti ya Utumishi wa Walimu (TSC) katika picha ya pamoja mara baada ya kufungua mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe hao tarehe 9 Septemba, 2024.

UONGOZI INSTITUTE YAWAFUNDA MENEJIMENTI
YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU

Baadhi ya Wajumbe wa Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu wakiwa katika mafunzo ya kujengewa uwezo kuhusu masuala mbalimali ya uongozi tarehe 9 Septemba, 2024 jijini Arusha.



Mratibu wa Mafunzo kutoka Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute), Emmanuel Tessua akitoa mada kuhusu akili tafukuri (Personal Leadership and Emotional Intelligence) wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo Menejimenti ya TSC tarehe 9 Septemba, 2024 jijini Arusha.



Mkufunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, Dkt. Ramadhan Marijani akitoa mada kuhusu uongozi wa Kimkakati (Strategic Leadership) wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo Menejimenti leo tarehe 9 Septemba, 2024 jijini Arusha.

KAMATI ZA TSC WILAYA ZATAKIWA KUZINGATIA SHERIA KATIKA KUTOA MAAMUZI



Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Jane Mtindya akizungumza katika mafunzo ya Wajumbe wa Kamati za TSC za Wilaya za Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini tarehe 25 Septemba, 2024 jijini Mbeya.

Na Mwandishi Wetu – Mbeya

Kamati za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) za Wilaya zimetakiwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu katika kufanya maamuzi mbalimbali yanayohusu utumishi wa Walimu ili kuhakikisha kila mwalimu anapata haki yake.

Kauli hiyo imetolewa na Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Jane Mtindya tarehe 25 OKTOBA 2024 akimwakilisha Mwenyekiti wa TSC katika Mafunzo ya Kamati za Tume hiyo kwa Wilaya za Kanda ya Nyanda za Juu kusini yanayofanyika kwa siku mbili jijini Mbeya.

Alisema kuwa Kamati za Wilaya zipo na zinafanya kazi kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 na Kanuni zake za mwaka 2016, hivyo wajumbe wake wanapaswa kufanya kazi na kutoa maamuzi kwa haki, kujiamini na kwa uhuru bila kuingiliwa na mtu au chombo chochote.

“Mpo katika nafasi hizo kwa

mujibu wa Sheria, hivyo mnapaswa kufanya kazi kwa kuzingatia sheria na siyo kwa kusukumwa na hisia. Mmepewa mamlaka ya kusimamia na kuamua masuala ya utumishi wa walimu katika wilaya zenu, msiyumbishwe katika kufanya maamuzi, msiamue kwa kumwonea au kumpendelea mtu,” alisema Kamishna Jane.

Akisisitiza kuzingatia sheria, Kamishna Jane aliwaeleza wajumbe hao kuwa sheria inamruhusu mwalimu kukata rufaa pale ambapo hajaridhika na maamuzi yaliyotolewa, hivyo Kamati zisipozingatia sheria siyo tu kwamba zitaharibu taswira njema ya TSC katika kutenda haki kwa walimu bali zinaweza kusababisha hasara kwa Serikali.

Pamoja na hayo, kiongozi huyo alisisitiza wajumbe hao kuweka mkazo katika kutoa elimu na kusaidia kusuluhisha masuala ya walimu ili kusaidia walimu kuepuka kujiingiza kwenye utovu wa nidhamu unaosababisha kuchukuliwa hatua na kupewa

adhabu mbalimbali ikiwemo kufukuzwa kazi.

Alisisitiza kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu haipo kwa ajili ya kuwafukuza kazi walimu huku akiweka wazi kuwa kuwepo kwa mashauri mengi ya nidhamu siyo sifa njema na wala siyo kigezo kuwa Kamati zinafanya kazi vizuri.

“Kuwa na kesi (mashauri) nyingi siyo ufanisi. Tutumie nafasi tulizopewa kuwasaidia walimu waendele kutekeleza majukumu yao vizuri. Tusifikirie kuwa kila wakati tunapaswa kuwafukuza kazi tu, tukumbuke tuna wajibu wa kuwalea walimu kila wakati ili waendele kuwa watumishi wazuri. Walimu bado ni wachache hawatoshelezi mahitaji ya shule zetu, hivyo ni vyema tuwasaidie ili wasipungue zaidi kwa kufukuzwa kazi.

Vilevile, aliwataka wajumbe hao kuwa mfano mzuri wa kuigwa kwa kuwa na maadili mazuri kwa kujiepusha na vitendo vinavyokwenda kinyume na maadili ikiwemo kujihusisha na masuala ya rushwa, unyanyasaji, uonevu nk.

“Nimalizie kwa kueleza kuwa pamoja na masuala mengine ya walimu mna jukumu la kusimamia nidhamu na maadili yao. Sasa ni lazima ninyi wenyewe muwe na maadili, haiwezekani unasimamia maadili wakati wewe mwenyewe huna maadili hayo. Tunapaswa kuhakikisha tunakuwa role model (mfano wa kuigwa) kwa wale tunaowasimamia.

Mafunzo hayo yanafanyika kwa Kamati zote za Wilaya za TSC nchini katika Kanda tano (5) ambapo Kitaifa yamefunguliwa na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mhe. Zainab Katimba (Mb) katika Ukumbi wa Karimjee jijini Dar es Salaam huku vituo vingine vikifuatilia ufunguzi huo kwa njia ya mtandao.

Kwa upande wa Nyanda za Juu Kusini, Mafunzo hayo yamehusisha Kamati za Wilaya kutoka Wilaya za Mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Rukwa na Ruvuma.

KAMATI ZA TSC WILAYA ZATAKIWA KUZINGATIA
SHERIA KATIKA KUTOA MAAMUZI

Mkurugenzi wa Kitengo cha Sheria wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wakili Richard Odongo akitoa maelezo wakati wa mafunzo ya Wajumbe wa Kamati za TSC za Wilaya za Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini tarehe 25 Septemba, 2024 jijini Mbeya.



Afisa Tawala Mkuu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Makao Makuu, Bibi Eliainenyi Mariki akiwasilisha mada kuhusu Muundo na Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu wakati wa mafunzo ya Wajumbe wa Kamati za TSC za Wilaya za Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini tarehe 25 Septemba, 2024 jijini Mbeya.



Baadhi ya washiriki wa Mafunzo ya Wajumbe wa Kamati za TSC za Wilaya za Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini yanayofanyika jijini Mbeya wakiwa katika mafunzo hayo.

DKT. NDUMBARO: WASHAURINI WALIMU KUSOMEA SHAHADA ZENYE MRENGO WA KAZI ZAO



Katibu Mkuu Mstaafu wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Dkt. Laurean Ndumbaro akitoa mada kuhusu uongozi katika utumishi wa umma wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Menejimenti ya TSC yaliyofanyika jijini Arusha hivi karibuni.

Na Mwandishi Wetu-TSC-Arusha

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeaswa kuwashauri walimu wanaopenda kujiendeleza kimasomo waendeleo kusomea kozi ambazo zinaendana na kada yao ya ualimu ambazo

zitawasaidia katika kupanda madaraja badala ya kusoma masomo nje ya taaluma yao ya awali.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Katibu Mkuu Mstaafu wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dkt. Laurean Ndumbaro wakati akitoa mada kuhusu

uongozi katika utumishi wa umma kwenye mafunzo ya kuwajengea uwezo Menejimenti ya TSC yaliyofanyika mjini Arusha.

“Mwalimu atakuwa na fursa nzuri ya kupanda vyeo ikiwa atajiendeleza katika kada ya Ualimu kutoka ngazi ya cheti kuendelea ngazi ya Stashahada, ngazi ya Shahada na hatimaye Shahada ya Uzamili kwani itamjenga kuwa mahiri katika fani yake. Changamoto iliyopo sasa ni walimu kukosa elimu ya kutosha ya kile wanachopaswa kusomea pale anapojiendeleza, unakuta mwalimu mwenye shahada anakwenda kuchukua Shahada ya Uzamili katika fani nyingine na anapomaliza masomo anataka abadilishwe kada, jambo ambalo haliwezekani,” alisisitiza.

Aidha, Dkt. Ndumbaro alisema kuwa ni vyema Walimu wakaelimishwa kuwa wanapokwenda kusomea Shahada nyingine pindi wanaporudi wakitaka kubadilishwa ili watumikie Kada nyingine itawabidi waanze na mshahara wa mtumishi anayeajiriwa kwa mara ya kwanza.

“Katika Utumishi wa Umma nchini mtumishi akiwa ameajiriwa kwa shahada fulani kisha akiwa ndani ya utumishi wake anakwenda kusomea shahada nyingine nje ya ile ya awali akimaliza masomo kisha atataka kubadili kada itabidi aanze na mshahara wa mtumishi anayeajiriwa kwa mara ya kwanza kwani hata kubaliwa kuendelea na mashahara wake aliokuwa nao kabla ya kubadilisha kada, vinginevyo aendelee na kada yake ya awali,” alisema.

Alisema kuwa kitendo cha mtumishi kubadili kada nje ya ile ya awali ambayo ameitumikia kwa muda mrefu kinaathiri utumishi wake ikiwa ni pamoja na mshahara na upandaji wa madaraja yake kwa wakati kwani anaweza kurudi nyuma.

DKT. NDUMBARO: WASHAURINI WALIMU KUSOMEA SHAHADA ZENYE MRENGO WA KAZI ZAO



Baadhi ya Wajumbe wa Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu wakiwa katika mafunzo ya kujengewa uwezo ya uongozi yaliyofanyika jijini Arusha hivi karibuni.



Katibu Mkuu Mstaafu wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dkt. Laurean Ndumbaro akiwa katika picha na washiriki wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Menejimenti ya TSC yaliyofanyika jijini Arusha hivi karibuni.



Matukio mbalimbali wakati wa mafunzo ya kurvajengea urwezo wajumbe wa Kamati za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi ya Wilaya yaliyohusisha wilaya za Mikoa ya Kanda ya Zirwa yaliyofanyika hivi karibuni jijini Mwanza.

TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC) YAAHIDI KUENDELEA KUTOA HUDUMA BORA KWA WALIMU

**Na Mwandishi Wetu - TSC-
ARUSHA**

Wajumbe wa Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeahidi kutumia mafunzo ya siku tatu waliyopatiwa na Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute) kuendelea kutoa huduma bora kwa wadau wao wakiwemo walimu kwa ajili ya maendeleo ya Tanzania.

Ahadi hiyo imetolewa hivi karibuni mjini Arusha na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama wakati akifunga mafunzo ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Menejimenti ya TSC katika masuala mbalimbali ya uongozi.

Mwl. Paulina alisema kuwa mafunzo waliyopata yamewawezesha kupata ujuzi katika maeneo mbalimbali na kuahidi kuwa ujuzi huo waliupata watautumia kikamilifu katika kuboresha utoaji wa huduma kwa walimu.

"Tuwashukuru sana wawezeshaji wetu kwa mada nzuri ambazo zimetufanya tutoke tofauti na vile tulivyoingia hapa ... Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu inavyoondoka leo baada ya mafunzo haya ni tofauti na Menejimenti iliyoingia kabla ya mafunzo," alisema.

Mwl. Paulina aliongeza kuwa watazingatia mambo yote waliyojifunza kwa ajili ya kuendelea kuwa viongozi wa kimkakati katika kuendeleza huduma kwa wadau wote kwa manufaa ya Taifa.

Alisema kuwa wataendelea kuitumia Taasisi ya Uongozi katika kuwajengea uwezo wa Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu wa Kada mbalimbali wakiwemo Makatibu Wasaidizi waliopo katika Wilaya zote hapa nchini.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akifunga mafunzo ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Menejimenti ya TSC yaliyofanyika hivi karibuni jijini Arusha.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama (katikati waliokaa) akiwa na Wajumbe wa Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) katika picha ya pamoja hivi karibni mara baada ya kufunga mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Menejimenti ya TSC.



Matukio mbalimbali wakati wa mafunzo ya kurvajengea urwezo wajumbe wa Kamati za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi ya Wilaya yaliyohusisha wilaya za Mikoa ya Kanda ya Kaskazini yaliyofanyika hivi karibuni jijini Arusha.



Matukio mbalimbali wakati wa mafunzo ya kurvajengea uwezo wajumbe wa Kamati za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi ya Wilaya yaliyohusisha wilaya za Mikoa ya Kanda ya Kati yaliyofanyika hivi karibuni mjini Tabora.

MWL. PAULINA ATOA MAFUNZO KWA WATUMISHI WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU(TSC) WILAYA YA ARUSHA

Na Mwandishi Wetu, TSC – ARUSHA.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama ametoa mafunzo kwa Watumishi wa Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Arusha kwa lengo la kuwaongezea ujuzi na ufanisi wa utoaji huduma kwa walimu katika eneo lao.

Ametoa mafunzo hayo hivi karibuni wakati wa ziara yake ya siku mbili katika Wilaya ya Arusha ikiwa na lengo la kuwajengea uwezo Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Arusha juu ya uboreshaji wa huduma kwa wadau.

Mwl. Paulina aliwasisitiza watumishi hao kuwa na uhusiano mzuri na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha ili waendeleo kushirikiana katika kuhakikisha kuwa walimu wanakuwa na mazingira mazuri na wanatimiza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi.

Aliwataka kuwa na utaratibu wa utunzaji mzuri wa nyaraka na kumbukumbu mbalimbali ikiwemo majalada binafsi ya Walimu ili pindi yanapohitajika yapatikane kwa urahisi.

Mwl. Paulina aliwataka viongozi wa TSC wa Wilaya hiyo kuhakikisha wanakamilisha usajili wa Walimu wa Ajira Mpya kwenye Mfumo wa TSCMIS pamoja na kuwahimiza walimu kujaza taarifa ya utekelezaji wa majukumu yao kwenye Mfumo wa PEPMIS.

Aidha, Katibu wa TSC aliwataka watumishi wa Wilaya ya Arusha kuhakikisha kila mwezi wanaboresha Rejesta za Usajili na Usahihi wa Tange ikiwemo kuweka orodha ya walimu waliohama, waliopanda vyeo , waliostafaafu na wale walioacha kazi.

Sanjari na hayo, Mwl. Paulina aliwataka watumishi hao kuwa na orodha ya Walimu waliothibitishwa kazini mwaka 2023/24 ikilinganishwa na waliostahili kuthibitishwa kazini 2023/24 na orodha ya walimu ambao hawakuthibitishwa kazini na kuwapa barua za kujulishwa kuongezewa muda wa matazamia au kusitishiwa ajira.

Alisema kuwa pia wawe na orodha ya Walimu waliowasilisha maombi ya kubadilishwa vyeo na waliobadilishiwa kwa mwaka 2023/24, walimu waliopandishwa vyeo kwa mwaka 2023/24 ikilinganishwa na waliokuwa na sifa za kupanda na wenye sifa za kupandishwa cheo 2024/25.

Mwl. Paulina aliwataka Watumishi wa TSC kuangalia kama kunakuwepo kwa uzingatiaji wa Mpango wa Mafunzo kwenye kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kuonyesha idadi na orodha ya Walimu waliopo masomoni ikiwa ni pamoja na Rejesta ya Walimu waliokwenda masomoni inayoonesha Jina, namba ya kituo, kozi, chuo na tarehe ya ruhusa na tarehe ya kumaliza masomo.

UZINGATIAJI WA UTARATIBU WA MASUALA YA MAADILI NA NIDHAMU



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa elimu kwa Watumishi wa Ofisi hiyo wa Wilaya ya Arusha hivi karibuni kwa lengo la kuwajengea uwezo ili waendeleo kutoa huduma bora kwa walimu.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Mwl. Paulina amewataka Watumishi wa Ofisi hiyo ngazi ya Wilaya kuzingatia taratibu wakati wa kushughulikia masuala ya maadili na nidhamu kwa walimu ili kuhakikisha kuwa haki inatendeka.

Alisema kuwa taratibu kama Uendeshaji wa Uchunguzi wa awali, Usahihi wa Uandishi wa Hati za Mashtaka ikionyesha tuhuma, kanuni iliyokiukwa na zitokane na Kanuni ya 11 na kuhakikisha kuwa Katibu Msaidizi amesaini hati ya mashtaka.

Mwl. Paulina aliongeza kuwa mambo mengine ni kuzingatia sifa katika uteuzi wa Kamati ya uchunguzi, uandaji wa Hadidu za rejea kwa usahihi, uhakiki wa barua za Wito kwenye uchunguzi na namna mtuhumiwa anavyofikishiwa taarifa ikiwa inamuonesha siku, mahali na muda ambao uchunguzi unafanyika na haki ya kuwakilishwa na kuwasilisha vielelezo, kama alitumiwa barua ya wito siku 7 kabla ya uchunguzi pamoja na njia zilizotumika kufikisha barua ya Wito.

Aliongeza kuwa lazima kuwepo kwa mwenendo wa uchunguzi, Taarifa ya Kamati ya Uchunguzi (Mashtaka, utetezi, hoja, ufupisho wa ushahidi, uchambuzi wa yaliyojiri mbele ya Kamati, maoni na mapendekezo, Wajumbe, tarehe ya kuwasilisha taarifa na saini za Wajumbe, usahihi wa adhabu zinazotolewa na uthibitisho wa kutuma barua za uamuzi kwa wahusika kwa wakati

Katika hatua nyingine Mwl. Paulina aliwataka Watumishi wa TSC ngazi ya Wilaya kuhakikisha wanaendelea kutoa elimu kwa walimu ili kupunguza makosa ya kinidhamu pamoja na kutatua changamoto mbalimbali za kiutumishi zinazowakabili.

MWL. PAULINA ATOA MAFUNZO KWA WATUMISHI WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU(TSC) WILAYA YA ARUSHA



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akihakiki utunzaji wa taarifa mbalimbali za walimu alipokuwa akitoa elimu kwa Watumishi wa Ofisi hiyo wa Wilaya ya Arusha hivi karibuni kwa lengo la kuwajengea uwezo ili waendelee kutoa huduma bora kwa walimu.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Watumishi wa Ofisi hiyo wa Wilaya ya Arusha hivi karibuni mara baada ya kutoa elimu iliyokuwa na lengo la kuwajengea uwezo ili waendelee kutoa huduma bora kwa walimu.



KAMATI ZA TSC ZA WILAYA ZATAKIWA KUTEKELEZA MAJUKUMU YAKE KWA HAKI



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Adolf Ndunguru wakati akifunga mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) za Wilaya tarehe 26 Septemba 2024 jijini Mbeya.

Na Mwandishi wetu – Mbeya.

Kamati za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) za Wilaya zimetakiwa kutekeleza majukumu yake ya kusimamia masuala ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kwa haki ili kuwa na walimu wenye maadili na wanaojituma katika kutoa elimu kwa wanafunzi.

Agizo hilo limetolewa na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Adolf Ndunguru wakati akifunga mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati za TSC za Wilaya tarehe 26 September, 2024 jijini Mbeya.

Kiongozi huyo alisema ili Kamati ziweze kutenda haki ni lazima zifahamu kwa kina majukumu yake pamoja Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia Utumishi

wa Walimu na Utumishi wa Umma ili ziweze kusaidia maendeleo ya Sekta ya Elimu hususan katika utumishi wa walimu.

“Ninatoa rai kwenu kuwa wakati mnatekeleza majukumu yenu na kwa kunufaika na mafunzo mliyopata, mwende mkatende haki. Ninaamini mmepata uelewa mkubwa juu ya uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utekelezaji wa majukumu yenu, ninawataka muendee kutekeleza majukumu yenu ya msingi ili kuhakikisha walimu wanatimiza wajibu na wanapata haki zao kwa maslahi ya maendeleo ya elimu na Taifa letu,” alisema Katibu Mkuu.

Vilevile, Bw. Ndunguru alimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mapinduzi makubwa

anayoyafanya katika Sekta ya Elimu kwa kuwezesha miradi mbalimbali kutekelezwa.

Pamoja na hayo, Kiongozi huyo aliipongeza Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu chini ya Katibu wake, Mwl. Paulina Nkwama kwa kuamua kuwajengea uwezo wajumbe hao wa kamati huku akiweka wazi kuwa mafunzo hayo yataongeza ufanisi katika kutoa huduma kwa walimu.

Alihitimisha kwa kutoa wito kwa wataanzania kujitokeza katika zoezi la kuboresha daftari la wapiga kura na kushiriki katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwezi Novemba mwaka huu.

Mafunzo hayo yalifanyika katika Kanda tano (5) ambapo Kitaifa yalifungwa jijini Mbeya huku vituo vingine vikifuatilia hafla hiyo mubashara kwa njia ya mtandao.

MWL. PAULINA ATOA MAFUNZO KWA WATUMISHI WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU(TSC) WILAYA YA ARUSHA



Mkurugenzi wa Kitengo cha Sheria wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wakili Richard Odongo akitoa maelezo wakati wa kufunga mafunzo ya Wajumbe wa Kamati za TSC za Wilaya za Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini tarehe 26 Septemba, 2024 jijini Mbeya.

Baadhi ya Washiriki wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) za Wilaya wakifuatilia hotuba ya kufunga mafunzo hayo tarehe 26 Septemba 2024 jijini Mbeya.



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Adolf Ndunguru (kushoto) akimsikiliza Mkurugenzi wa Kitengo cha Sheria wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wakili Richard Odongo wakati wa kufunga mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) za Wilaya tarehe 26 Septemba 2024 jijini Mbeya.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Adolf Ndunguru (kushoto) akiagana na mmoja wa Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Jane Mtindya mara baada ya kufunga mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) za Wilaya tarehe 26 Septemba 2024 jijini Mbeya.



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Adolf Ndunguru (katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya washiriki wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) za Wilaya wakati wa hafla ya kufunga mafunzo hayo iliyofanyika tarehe 26 Septemba 2024 jijini Mbeya.

PROF. MURUKE: MAFUNZO MLIYOPATA YAKAWASAIIDIE KUTEKELEZA MAJUKUMU YENU KWA WELEDI



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Muruke akizungumza hivi karibuni na Wajumbe wa Kamati za Wilaya wakati wa mafunzo ya siku mbili waliyopata katika kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa weledi ili kupunguza rufaa zinazokatwa kutoka kwao kwenda ngazi za juu.

Na Mwandishi wetu -TSC- Dar es Salaam.

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu Prof. Masoud Muruke amewataka Wajumbe wa Kamati za Wilaya kutumia mafunzo ya siku mbili waliyopata kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa weledi ili kupunguza rufaa zinazokatwa kutoka kwao kwenda ngazi za juu.

Ametoa kauli hiyo hivi karibuni wakati wa kuhitimisha mafunzo ya siku mbili ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati za Wilaya za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Alisema kuwa mada walizofundishwa ikiwemomuundo na majukumu ya Tume, Majukumu ya Kamati za Wilaya pamoja na taratibu katika ushughulikiaji wa

mashauri ya nidhamu na Rufaa kwa Walimu zitawawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyopo.

“Mafunzo yamekuwa na maana sana kwa washiriki wote ikiwa ni pamoja na mimi baada ya elimu hii ya siku mbili kuna kitu nimeongeza. Natumaini mtatekeleza majukumu yenu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na kuepuka makosa mabaya yamesababisha rufaa ambazo wakati mwingine zinapofika juu Warufani wanashinda kwa makosa ambayo yametokana na kutozingatia sheria na taratibu,” alisema.

Alisema kuwa makosa ambayo yamekuwa yakitokana na baadhi ya Wajumbe wa Kamati za Wilaya kutozingatia Sheria, Kanuni na Taratibu wakati mwingine yamekuwa yakisababisha hasara

kwa Serikali.

Prof. Muruke alisema kuwa ni vyema wakatamia mafunzo hayo katika kuhakikisha kuwa kama kuna mtu ameshitakiwa na hana hatia anapewa haki yake na yule mwenye hatia anawajibika kwa makosa yake.

Mafunzo hayo ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati za Wilaya yamefanyika katika Kanda mbalimbali ambapo Kanda ya Kaskazini ilihusisha mikoa ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro na Tanga; Kanda ya Mashariki ilihusisha mikoa ya Lindi, Mtwara, Dar es Salaam, Pwani na Morogoro; Kanda ya Kati ilihusisha mikoa ya Kigoma, Katavi, Tabora, Singida na Dodoma; Kanda ya Ziwa mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Geita; na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini mikoa ya Rukwa, Songwe, Ruvuma, Njombe, Iringa na Mbeya.

TSC YAPONGEZA JITIHAHA ZA RAIS SAMIA SULUHU HASSAN KATIKA KUBOresha SEKTA YA ELIMU



Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Jane Mtindya akitoa neno la utangulizi wakati wa hafla ya kufunga mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati za TSC za Wilaya tarehe 26 September, 2024 jijini Mbeya.

Na Mwandishi Wetu – Mbeya.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imepongeza jitihada zinazofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kusimamia maendeleo ya Sekta ya Elimu hususan kwa walimu.

Pongezi hizo zimetolewa na Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Jane Mtindya akitoa neno la utangulizi kwa niaba ya Mwenyekiti wa TSC, Prof. Masoud Hadi Muruke wakati wa hafla ya kufunga mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati za TSC za Wilaya tarehe 26 September, 2024 jijini Mbeya.

Alisema kuwa Rais Samia

amefanya kazi kubwa kuhakikisha walimu wanapata haki zao ikiwa ni pamoja na kupandishwa vyeo kwa wakati, kubadilishiwa vyeo kwa wale wenye sifa pamoja na kuendelea kulipa madeni mbalimbali yakiwemo ya uhamisho, likizo na malimbikizo ya mishahara.

“Serikali ya Awamu ya Sita imefanya mambo makubwa kwa ajili ya walimu, tunashukuru kwamba walimu wanapandishwa madarajakwa wakati namwakahuu tumeona wengi wamepandishwa kwa mserereko jambo ambalo hatukuwahi kulishuhudia,” alisema.

Pia, Kamishna huyo alieleza kuwa Serikali inayoongozwa na Rais Samia imeendelea kuboresha miundombinu mbalimbali ikiwemo ujenzi wa vyumba vya

madarasa, maabara, ukarabati wa shule pamoja na ujenzi wa nyumba za walimu jambo ambalo limesaidia walimu kufanya kazi katika mazingira bora zaidi.

“Sambamba na hilo, tumeona miradi mbalimbali ikielekezwa kwa walimu ikiwemo mradi wa kuimarisha shule za msingi (BOOST) na mradi wa kuimarisha shule za sekondari (SEQUIP). Pamoja na mambo mengine, katika miradi hiyo walimu wameendelea kupata mafunzo mbalimbali ili waweze kufundisha wanafunzi kwa ufanisi zaidi,” alisema.

Akizungumzia maendeleo ya Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Jane alisema kuwa kitendo cha Serikali kuruhusu fedha zitumike kwa ajili ya kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati za Wilaya ni ishara kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inawajali sana walimu na inataka TSC itoe huduma inayokidhi matarajio ya walimu.

Vilevile alieleza kuwa TSC imeendelea kuongezewa bajeti huku fedha nyingi zikielekezwa katika kushughulikia masuala ya walimu, alieleza kuwa kila ofisi ya Wilaya imepatiwa pikipiki na wilaya tisa (9) zimepatiwa magari kwa lengo la kuwafikia walimu kwa urahisi na kuweza kutatua changamoto zao.

“Ndugu Katibu Mkuu, tuna jengo la Ofisi ya TSC Makao Makuu linalojengwa pale Dodoma, jengo hilo linagharimu shilingi bilioni 6.4 na kwa sasa ujenzi unaendelea, tunaamini jengo hilo litakamilika kwa wakati ili walimu wetu waweze kuhudumiwa vizuri na watumishi Tume wawe na mahali pazuri pa kufanyia kazi. Haya yote yanatokea kutokana na jitihada za Rais wetu za kuhakikisha walimu wanapata huduma iliyo bora,” alihitimisha.

Mafunzo hayo yalifungwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Adolf Ndunguru.

**PROF. MURUKE: MAFUNZO MLIYOPATA YAKAWASAIIDIE
KUTEKELEZA MAJUKUMU YENU KWA WELEDI**

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Masoud Muruke akizungumza hivi karibuni na Wajumbe wa Kamati za Wilaya wakati wa mafunzo ya siku mbili waliyopata katika kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa weledi ili kupunguza rufaa zinazokatwa kutoka kwao kwenda ngazi za juu.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu